



Mafunzo ya ualimu

Utangulizi

Programu za Mafunzo ya Ualimu ndiyo moyo wa mifumo ya elimu kwani huweka msingi wa ujuzi na maarifa ambavyo ndiyo tegemeo kwa walimu wapya darasani¹ wakishaajiriwa. Hivyo, programu kubwa za namna hii zinazolenga katika kujenga Msingi wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwenye ngazi ya skuli za msingi katika nchi za kipato cha chini na cha kati, lazima ziweke mkazo katika kuwaandaa walimu tarajali ili kuhakikisha panakuwepo na uendelevu wa upatikanaji wa nguvu kazi bora ya walimu. Programu hizi badala yake zimekuwa zikijikita zaidi katika mafunzo ya walimu kazini kwa mtazamo wa kuwa, kufanya hivyo kutakuwa na matokeao chanya na ya haraka kwa upande wa wanafunzi. Hivyo, matokeo yake imekuwa Programu za Elimu ya Ualimu zimekuwa mara kwa mara haziendani na kile kinachofanyika darasani, hii ikiwa na maana kwamba walimu wapya kutoka vyuoni wanaojirriwa wanakuwa hawana ujuzi unaohitajika kutekeleza programu ya KKK. Ili kuepuka tatizo hili, hapana budi kuimarisha programu za elimu ya ualimu, sambamba na mabadiliko ya sera zinazohusiana na uchaguzi wa waombaji kuijunga na programu za mafunzo ya ualimu na upangaji wa wahitimu wa ualimu katika skuli ili uzingatie masomo yao.

FASILI ZA MANENO YA MSINGI

Mazoezi ya ufundishaji kwa Vitendo: Mazoezi ya kufundisha, ambayo kwa kawaida hufanyika karibu na mwisho wa programu ya mafunzo ya ualimu

Uchaguzi: taratibu na shughuli zinazotumika kuwawutia waombaji wa programu za mafunzo ya ualimu

Upangaji: mchakato wa kuwasambaza walimu wenyi sifa (wapya na wazoefu) katika skuli. Mchakato huu unaweza kufanya na serikali kuu au ngazi ya ngazi ya skuli au Ngazi ya wilaya.

Mafunzo kabilishi: Programu za mafunzo kazini zenyi lengo la kutoa mafunzo ya kukabiliana na mazingira mapya ya kazi kwa walimu wapya kuhusu utendaji kazi, sera na mbini za ufundishaji na ujifunzaji zinazotumika katika skuli

MADHUMUNI YA MWONGOZO HUU

Katika Mwongozo huu tunatoa mapendekezo kwa watunga sera, wafadhili, watekelezaji na wafundishaji walimu kuhusu namna bora ya kuendeleza Elimu ya Ualimu wa ngazi ya skuli ya msingi ili kujenga KKK. Tunajadili suluhisho muhimu kwa changamoto zinazohusiana na mitaala, Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo katika maskuli (Yale ya muda mrefu), Mahitaji ya Mafunzo endelevu kazini kwa wafundishaji walimu wa programu za Elimu ya Ualimu. Uchaguzi wa wanachuo katika programu za ualimu na sera za upangaji wa walimu wapya katika vituo vya kazi (katika skuli). Tunatoa ushahidi kutoka katika nchi za kipato cha chini na kati, na kutoka katika nchi za kipato cha juu pale tunapoona inawezekana na unafaa. Tunaonesha ni kwa jinsi gani elimu ya ualimu ni muhimu kwa ujumla wake hasa katika kumwendeleza mwalimu. Kuanzia katika udahili wa programu ya ualimu inayohusika (hatua ya 1) mpaka katika kupangiwa ajira mpya (hatua ya 4) na kushiriki katika programu za mafunzo kabilishi (hatua ya 5). Ili Programu za KKK zifanikiwe zinapaswa kuzingatia hatua zote za uendevezaji wa mwalimu. Hivi sasa, programu nydingi za KKK zimejikita tu katika hatua 6 na 7, tafsiri yake ni kwamba fursa kadhaa na muhimu zinazoweza kuwa na ushawishi na zenye kuhitaji uboreshaji zimekuwa zikifujwa. Mwongozo huu ni matokeo ya mapitio ya kina ya maandiko mbalimbali yanayochambua kwa kina maandiko ya sasa na upungufu uliopo katika maarifa yanayohusu uandaaji wa walimu katika nchi za kipato cha chini na cha kati.

KIELELEZO 1. Mwendelezo wa ukuaji wa mwalimu kitaaluma na kitaalamu



MAFUNZO YA UALIMU (MyU)

MAFUNZO ENDELEVU KAZINI NA MSAADA ENDEELEVU



Mafunzo ya Ualimu: Muundo na Mtaala

Muundo wa Mafunzo ya Ualimu unatafautiana sana kati ya nchi moja na nyingine.² Nchi za kipato cha juu, na zenyetendaji wa juu zinazoshiriki katika Programu ya upimaji wa wanafunzi wa kigeni (PISA) zinaprogramu za Mafunzo ya Ualimu zenyet kuanzia muda wa miaka mitatu (Flanders, Ubelgiji), hadi miaka saba (Ujerumanji).³ Katika nchi zenyet kipato cha chini na cha kati, mafunzo ya Ualimu huchukua kuanzia miaka miwili hadi mitatu, kama iliyokuwa kwa Stashahada ya Ualimu wa kiwango cha msingi; miaka mitatu nchini Zambia, na miaka miwili kwa Stashahada ya ualimu nchini India. Hata hivyo, wakati mwingine Mafunzo ya ualimu huchukuamuda mfupi zaidi. Huko Nepal, elimu ya sekondari ya juu inayotolewa kwa miezi kumi inatosha kumfanya muhitimu kuwa na sifa ya kuwa mwalimu wa skuli ya msingi, wakati Taasisi za Sri Lanka hutoa Stashahada ya ualimu kwa muda wa mwaka mmoja.⁴

Ni kawaida kwa aina mbalimbali za mafunzo ya ualimu kutolewa katika nchi mbali mbali. Kwa mfano, vyuo vikuu vinaweza pia kutoa Shahada za Ualimu, pamoja na programu fupi za mafunzo ya Ualimu zinazotolewa na vyuo vya kati na vyuo vya ufundi stadi. Kwa kawaida Shahada huhitajika zaidi kwa ajili ya walimu wa sekondari kuliko kwa walimu wa skuli za msingi, ingawa nchi nyingi za kipato cha kati, ikiwa ni pamoja na Jordan, Morocco, Thailand, na Georgia, pia wanazihitaji kwa ajili ya walimu wa skuli za msingi. Katika miaka ya hivi karibuni, baadhi ya nchi za kipato cha chini na cha kati zimeongeza muda na viwango vya Shahada vinavyohitajika kwa elimu ya Ualimu ili kuendana na viwango vya uandaaji wa walimu katika nchi zenyet utendaji wa juu⁵ (pamoja na Myanmar; tazama kisanduku). Kiunzi cha sifa ya mwalimu cha Umoja wa Afrika⁶ kinaleza kwamba kiwango cha chini cha elimu ya mwalimu kwa sasa kinapaswa kuwa Shahada ya elimu, ingawa hili bado halijatekelezwa sana katika nchi wanachama kwa sababu ya changamoto zinazohusiana na ghamrama na vifaa. Hivi karibuni, Ghana imeanza kutoa Shahada za ualimu katika vyuo vyake; hapo awali mtu alikuwa akiweza kuwa mwalimu kwa kupata stashahada ya ualimu ya muda wa miaka mitatu.

Kwa ujumla, mifumo pia inatofautiana sana kulingana na aina za waombaji wanaovutiwa na ualimu kama taaluma na kwa programu za mafunzo ya ualimu. Nchini Ethiopia, kwa mfano, wanafunzi wanawenza kuingia katika programu za mafunzo ya ualimu baada ya kumaliza Kidato cha Nne ikiwa hawajafuzu kuendelea na elimu ya sekondari ya juu, kulingana na alama zao za mtihani wa taifa.⁹ Mitindo hii ina athari kubwa kwa aina za waombaji wa programu za ualimu na mwelekeo wa mtaala katika programu hizo, kama inavyoelezwa zaidi hapa chini

Bila kujali muda na muundo wake, programu za mafunzo ya ualimu zinapaswa kubuniwa kwa kuhusisha nadharia na uhalisia wa utendaji.¹⁰ Licha ya kwamba hakuna mtaala rasmi wa mafunzo ya ualimu, **walimu wapya wanahitaji kuelewa maudhui ya masomo wanayofundisha (maarifa ya maudhui) na jinsi ya kufundisha vyema kwa ujumla, ikijumuisha usimamizi wa darasa na ushirikishaji wa wanafunzi katika kujifunza (ujuzi wa mbinu za kufundishia).**¹¹ Maudhui ya mtaala wa mafunzo ya ualimu lazima yafafanuliwe na kile ambacho walimu katika muktadha fulani wanawenza kukifanya, na yanapaswa kuzingatia ufundishaji wa kiwango cha juu (yaani, mbinu za ufundishaji ambazo ni muhimu kwa kuimarisha matokeo ya ujifunzaji kwa wanafunzi wote na kuendeleza ujuzi wa kufundishaji).¹² Mtaala unapaswa kuandaliwa ili kuendana na viwango vyoyote vya kitaifa vya walimu wa skuli za msingi. Walimu tarajali katika nchi za kipato cha chini na cha kati wanahitaji kutayarishwa kwa ajili ya kufundisha madarasa makubwa na madarasa yenye kuwa na mchanganyiko wa ngazi tafauti, wanafunzi walio na umri mkubwa zaidi, wanaozungumza lugha zaidi ya moja na, mara nyingi, wanafunzi wasiokuwa na msingi wa stadi za KKK. Sasa hivi, kuna ushahidi mdogo kuhusu uhusiano kati ya vipengele vya mtaala na matokeo ya ujifunzaji ya walimu tarajali katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Hata hivyo, ushahidi kutoka nchi za kipato cha juu hutoa ufahamu juu ya umuhimu wa uhusiano wa **maarifa ya Hisabati** kwa walimu na ufaulu wa wanafunzi wa matokeo ya kujifunza.¹³

Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Ualimu nchini Myanmar (STEM)

Myanmar inafanya mageuzi katika mafunzo ya ualimu kwa msaada wa kifedha kutoka kwa serikali za Australia, Finland, na Uingereza na msaada wa kitaalamu kutoka UNESCO. Mfumo wa elimu ya ualimu wa nchini hii umeboreshwa hadi kufikia programu ya miaka minne na kuwiana na viwango vya kimataifa. Kwa mara ya kwanza ulatekelezwa katika mwaka wa masomo 2019/2020, mtaala mpya wa ualimu unajumuisha mihutasiari ya masomo, vitabu vya kiada, na miongozo ya ufundihaji ya waelimisha walimu. Waelimisha walimu wamepatiwa maelekezo ya utekekelezaji na mafunzo kwa zaidi ya 98%. Watathmini wamegundua kwamba “Wakufunzi wanatumia miongozo ya kufundishia kuandaa karibu kila somo.⁸





Nchi za kipato cha chini na cha kati zinakabiliwa na changamoto nyingi zinazohusiana na maudhui ya mtaala ya mafunzo ya ualimu. Katika programu nyingi za sasa za mafunzo ya ualimu, shughuli za upimaji endelevu zinaweka msisitizo zaidi katika maarifa ya maudhui kuliko mbinu za kufundishia, na kujikita zaidi katika nadharia kuliko vitendo.¹⁴ Licha ya msisitizo huu kuwekwa kwenye maarifa, mafunzo ya ualimu yameshindwa kuwawezesha walimu tarajali kufikia viwango stahiki vya umahiri wa maudhui hayo.¹⁵ Katika nchi nyingi za kipato cha chini na cha kati, programu za mafunzo ya ualimu kwa kawaida hudahili wanafunzi ambao walikosa udahili katika programu zenye kuwa na ushindani zaidi na za kuvutia waombaji wengi katika ngazi ya elimu baada ya sekondari.¹⁶ Matokeo yake, walimu wengi wanahitaji kufanya kazi ya ziada ili kupata maarifa ya maudhui mahususi ya masomo wanayofundisha.

Changamoto nyengine ni kwamba mifumo mingi ya elimu ya msingi inaelekeea katika kuwashirikisha zaidi wanafunzi katika ujifunzaji wao badala ya kuwafanya wafyonze maarifa kutoka kwa walimu. Ingawa programu nyingi za hivi karibuni zinahusiana na ujenzi wa msingi wa KKK katika nchi zenye uchumi wa chini na wa kati zimeanzishwa ili ziwe na mwilingiliano na haraka zaidi katika kukuza stadi za wanafunzi, programu za mafunzo ya ualimu zimeendelea kujikita katika ufundishaji kwa njia ya muhadhara.¹⁷ **Kwa hiyo, walimu tarajali wanapewi nafasi ya kuona na kufanya mazoezi ya ufundishaji yenye ufanisi, kuweka katika vitendo njia za ufundishaji, na hatimaye kuja kufundisha kwa jinsi ambayo walifundishwa.**

MAPENDEKEZO

- 1 Kuandaa walimu tarajali kwa ajili ya madarasa halisi. Mtaala wa mafunzo ya ualimu uwe ni wenye kuhusiana moja kwa moja na matarajio ya kile ambacho walimu wanapaswa kufanya darasani,** hasa katika madarasa ya kujenga msingi wa KKK. Kama inavyooneshwa katika Kielelzo 1, Mafunzo ya Ualimu ni hatua moja tu katika mwendelezo wa kuandaa walimu bora wa viwango vya juu, na hatua zote zinahitaji kuwiana. Hii ina maana kwamba watunga sera lazima wazingatie uendelezaji wa mwalimu katika viwango vya kitaifa na kikanda, mtaala ya elimu ya msingi, programu za mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya walimu wapya, na mafunzo kazini kwa ujumla na hasa ya kujenga msingi wa KKK.¹⁸
- 2 Kujumuisha kozi za msingi katika mitaala ya elimu ya ualimu.** Mitaala ya elimu ya ualimu **inatakiwa kuwa na kozi za msingi zenyne maudhui ya KKK na ujuzi wa ufundishaji** ili kuhakikisha ufundishaji wa sasa, mikabala ya ushahidi ya ufundishaji wa KKK. Walimu wote wa KKK wanapaswa kuchukua kozi katika mkabala wa jumla wa Ujifunzaji. Aidha, kanuni za mkabala wa jumla wa ufundishaji zinapaswa kuingizwa katika kozi za programu za mafunzo ya ualimu ili kuhakikisha kwamba walimu tarajali wanajengewa uwezo wa kushughulikia mahitaji ya kitaaluma, kijamii na kihisia ya wanafunzi mbalimbali watakaokutana nao. Kwa upande wa kusoma na kuandika, kwa uchache misingi ya mbinu za kufundishia kusoma, ufundishaji unaoongozwa na tafiti kuanzia ngazi ya neno hadi ngazi ya matini, uingizaji wa kusoma na kuandika, upimaji msingi wa mwanafunzi, ufundishaji unaozingatia mahitaji ya mwanafunzi. Kwa upande wa Hisabati, mada za msingi zinapaswa kujumuisha kusoma nambari na matendo, aljebra, jometri, na vipimo na takwimu kupitia mkabala unaochanganya maarifa ya maudhui¹⁹ na maarifa ya mbinu za kufundishia. Aidha, walimu tarajali wanapaswa kuandaliwa kutumia teknolojia sahihi na kwa kuchagua vifaa na nyenzo za kuwezesha ujifunzaji. Programu za mafunzo ya ualimu zinapaswa pia kujumuisha nyenzo halisi za kufundishia KKK zinazotumika kote nchini, kwa hivyo walimu tarajali wanakamilisha mafunzo yao ya ualimu wakiwa tayari na uwezo wa kufundisha programu mahususi za KKK zilizopo.

- 3 Kuhusisha nadharia na vitendo. Mtaala unapaswa kuchanganya nadharia ya kufundishia na ufundishaji darasani** badala ya kuvigawanya katika kozi tafauti.²⁰ Hii inaweza kuhusisha ufundishaji kiduchu, shughuli za video, kufundisha watoto wa madasa ya awali wenye uwezo mdogo na walio katika skuli za jirani, kuchunguza kazi za wanafunzi sambamba na za mwalimu, kujadililiana na walimu tarajali wa ngazi ya juu zaidi na wahitimu wa hivi karibuni, na kuwatizama walimu mahiri wanaohusisha na mtaala wa taifa.²¹ Uzoefu huu unaotumika pia unaweza kusaidia katika ukuaji wa kitaalamu miongoni mwa walimu tarajali, kuimariswa zaidi wakati hatua ya mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo.





Kuanzisha Mazoezi Bora ya Kufundisha kwa Vitendo

Mazoezi ya Kufundisha kwa vitendo ni moja ya hatua katika Mafunzo ya ualimu chuoni, ambapo mwalimu tarajali anafundisha akiwa chini ya usaidizi wa mwalimu mzoefu wa skuli inayohusika. Muundo, muda na urefu wa mazoezi ya kufundisha kwa vitendo hutafautiana katika nchi mbali mbali;²² upangaji skuli unaweza kuwa mfupi kama wiki chache au muda mrefu kama mwaka wa masomo. Utafiti kutoka nchi za kipato cha juu na cha kati umehusisha uzoefu wa ufanisi wa mazoezi ya kufundisha kwa vitendo na walimu kujisikia kuwa tayari zaidi kufundisha,²³ kukuza utambulisho wa kitaaluma,²⁴ na kuelewa vizuri umaskini na changamoto za kimuktadha zinazopatikana katika skuli.²⁵ **Uzoefu thabiti wa mazoezi ya kufundisha ni fursa ya kujenga mielekeo ya kitaaluma, ambayo ni “mielekeo ya kitaalamu, maadili, na imani zinazodhahirisha lugha na matendo pale wakufunzi wanakutana na wanafunzi, familia, wafanyakazi wenza na jamii.”**²⁶ Iwapo walimu tarajali watapata mwongozo wa wazi kuhusu tabia na mielekeo yao wakati wa mazoezi yao ya kufundisha kwa vitendo, itawasaidia hapo baadaye katika maisha yao ya kazi ya ualimu

Katika nchi za kipato cha chini na cha juu, kumebainika mfululizo wa changamoto zinazohusiana na mazoezi ya kufundisha kwa vitendo. Kwanza, muda wa mazoezi ya kufundisha mara nyingi ni mfupi sana,²⁷ hii ni kutokana na tafiti za hivi karibuni zinazonesha mazoezi ya muda mfupi ya wiki mbili katika programu ya mafunzo ya ualimu ya miezi tisa.²⁸ Pili, walimu tarajali mara nyingi hupata usimamizi na mrejesho kidogo na hafifu kutoka kwa walimu wakufunzi wakati wa mafunzo yao ya ualimu chuoni.²⁹ Tatu, Mara nyingi uzoefu wa mazoezi ya ufundishaji skuli umedhahirisha tafauti zilizopo kati ya kinachofundishwa katika kozi za ualimu chuoni na uhalisia wa kinachotendeka skuli, walimu wanasihii wakati mwingine hutumia mikabala ya ufundishaji isiyoundana na njia za ufundishaji zilizomo kwenye mtaala wa ualimu. Nne, mara kwa mara walimu tarajali hujichagulia maeneo yao ya kufanya mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo, hii husababisha zoezi la ufundishaji kwa vitendo kufanya kwa kuchagua kilichokuwa rahisi kuliko ubora wa skuli na mwalimu mnasihi.

MAPENDEKEZO

Mapendekezo yenyewe ushahidi hapa chini ni matakwa ya shabaha ambazo programu za mafunzo ya ualimu katika muktadha wowote ule zinaweza kufanya kazi kwa muelekeo huo. Ingawa kufanikiwa kikamilifu kwa malengo haya kunaweza kuchukua muda mrefu hasa panapokuwepo na rasilimali chache, hatua ndogo ndogo zinazopigwa kuelekea ufikiaji wa malengo hayo zinathabitisha maendeleo mazuri.

- 1 Kuwapanga walimu tarajali katika vituo vya kufanya mazoezi ya muda mrefu ya ufundishaji kwa vitendo kwa kuzingatia malengo** Vyuo vya ualimu viwapange wanachuo wao katika skuli zenye ubora na zinazoendeshwa vizuri³⁰ zenye walimu wanasihii wenyewe kutambua jukumu lao kuwa ni kutoa fursa za unasihi kwa walimu tarajali, badala ya kuwatumia kama mbadala wao. Pale inapowezekana walimu tarajali wapatiwe posho za kujikimu kwa ajili ya makazi na gharama za maisha badala ya kuwapangia katika skuli zilizo jirani na nyumbani kwao.
- 2 Inahitajika kuwa na kiwango cha chini cha muda wa mazoezi ya muda mrefu ya ufundishaji kwa vitendo** Nchi zinapaswa **kupanga muda wa chini kabisa kwa ajili ya mazoezi ya muda mrefu ya ufundishaji kwa vitendo na kusimamia utekelezaji wa viwango hivyo.** Wiki chache hazitoshi kumjenga mwalimu tarajali kuwa mwalimu mahiri. Hata hivyo, kuna uwiano kati ya urefu wa muda wa mazoezi ya muda mrefu ya ufundishaji kwa vitendo na gharama ya programu ya mafunzo ya ualimu iliyoongezwa muda wake, hususani pale ambapo pana upungufu wa walimu wanasihii na rasilimali zinazopatikana kwa ajili ya walimu tarajali hasa wakati kuna upungufu wa walimu wasaidizi waliohitimu na rasilimali zinazopatikana kwa ajili ya makazi ya walimu tarajali jirani na skuli, au kuwapatia usafiri wa kwenda skuli na kurudi nyumbani.³¹
- 3 Kuimarisha mazoezi ya muda mrefu ya ufundishaji kwa vitendo.** Mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo lazima yaandaliwe kwa namna ambayo yanaruhusu **kukua kwa uhuru wa walimu tarajali**, kukua kwa uhuru wa walimu tarajali, yawape fursa walimu tarajali kutenda kile walichojifunza chuoni.³² Walimu wanasihii wakati mwengine hupata ugumu wa kuwapa uhuru walimu tarajali kwa kuhofia kurudia kufundisha mada hizo baadaye.³³ Hata hivyo, walimu tarajali hawapaswi kumaliza mazoezi yao ya muda mrefu ya kufundisha kwa vitendo bila ya kupatiwa fursa ya kufundisha kwa uhuru- kufanya mazoezi ya kuandaa maandalio ya masomo, kufundisha, kupima wanafunzi na kutathimini utendaji wa kila mmoja wao.
- 4 Kusisitiza kufanya mazoezi ya tafakuri** Shughuli zinazohitajika wakati wa mazoezi ya muda mrefu ya ufundishaji kwa vitendo zinapaswa kuwa zile **zinazompelekea mwalimu tarajali kutafakari na kujitathmini**,



kama vile kutunza kumbukumbu zake na kujadiliana na walimu tarajali wenzake.³⁴ Shughuli hizi zitaweza kufanyika iwapo kutakuwa na usaidizi kutoka kwa wakufunzi wa walimu na walimu wanasihi.

- 5 Kupata mrejesho bora kutoka kwa walimu wanasihi.** Walimu tarajali wanahitaji kupatiwa **mrejesho bora na wa mara kwa mara kutoka kwa walimu wanasihi.** Mrejesho bora ambao unawasaaidia, unawajenga, uko wazi, ni wa kiuchunguzi, unaowafanya watafakari kwa kina na unawapa mafanikio ya ubora katika ufundishaji.³⁵ Mwalimu mnasihi anapaswa kuwa ni mwenye kutoa na kujitolea mara kwa mara kwa kufanya kazi isiyokuwa na malipo na yenye changamoto ya usimamizi na utoaji wa mrejesho kwa walimu tarajali kuhusu mazoezi yao ya ufundishaji. ³⁶ Walimu wanasihi wanapaswa kupatiwa mafunzo juu ya utekelezaji wa jukumu hili gumu. Nchini Kenya, Mradi wa TUSOME wa Kusoma na Kuandika (KK) unafanya kazi na Wizara ya Elimu katika kuandaa upya vigezo nya tathmini nya mazoezi ya kufundisha kwa vitendo ili kuendana na jinsi ya kuwatathimini walimu tarajali kuhusu uwezo wao wa kufundisha stadi za KKK kwa ajili ya kutekeleza kwa ufanisi programu za KKK katika skuli.

6 Kushirikiana kikamilifu na skuli jirani kwa kubadilishana uzoefu ili kukuza ubora wa maeneo ya kufanya mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo Ili kufikia

Pendekezo la 1, **programu za ualimu lazima zifanye kazi na skuli za maeneo ya jirani ili kuwaandaa walimu wanasihi ikiwemo kutayarisha mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo kwa kushirikiana.**³⁷ Ili kufikia ubora wa hali ya juu, maeneo ya mazoezi ya ufundishiaji kwa kivitendo, uhusiano kati ya programu za mafunzo ya ualimu na skuli, unapaswa kuwa mzuri kwa pande zote; kuwa na matarajio mahsus kwa walimu, wakufunzi wa walimu, walimu wanasihi, na walimu tarajali; na kuhakikisha kuwepo kwa manufaa kwa pande zote.³⁸ Aidha, skuli ya mazoezi lazima ichukuliwe kuwa ni eneo la ujifunzaji, ambapo skuli nzima, na sio tu mwaliimu mnasihi ndiye mwenye jukumu la kuwasaidia walimu tarajali.³⁹ Hata hivyo, shughuli hizi ili ziwe endelevu zinahitaji uwezo wa kifedha.⁴⁰

Kumsaidia Mkufunzi wa Walimu na Taasisi katika Utoaji wa Mafunzo ya Ualimu

Wakufunzi wa walimu ni wahusika muhimu katika juhudzi za kuimarishe ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Walimu tarajali wataimarishe mbinu zao za ufundishaji kulingana na mbinu walizoelimishwa wao katika mafunzo yao.⁴¹ Maarifa yanayotolewa na wakufunzi wa walimu yanajenga msingi katika maarifa ambayo walimu tarajali watayatumia. Mafunzo yanayotolewa na wakufunzi wa walimu huwajengea msingi mpya walimu tarajali.⁴² Kama ilivyooneshwahapo juu, hata hivyo, wakati mtaala ya skuli za msingi inazidi kumfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji, programu za mafunzo ya ualimu bado zimeendelea kubaki kumfanya mkufunzi wa walimu kuwa ndiye kitovu cha ujifunzaji. Wakufunzi wa walimu hawana fursa kubwa za kujihusisha na ufundishaji wa sasa unaofanya katika skuli za msingi, kwa kuwa kwa ujumla programu nyingi na kubwa zimejikita katika kuwajengea uwezo walimu wa skuli za msingi kufundisha stadi za KKK. Hii inaweza kusaababisha imani na mikabala kinzani mionganoni mwa walimu wapya.⁴³

Katika nchi za kipato cha chini na za kipato cha kati, mara nyingi wakufunzi wa walimu hukosa maarifa ya maudhui ya masomo wanayofundisha, na maarifa ya mbinu za kufundishia kwa ujumla na maarifa ya mbinu za kufundishia mahususi kwa masomo wanayoyafundisha, na hivyo kuishia kutegemea sana mbinu ya muhadhara katika ufundishaji wao. Maandalizi yao ya ufundishaji yamepitwa na wakati, na wanafanya kazi katika mazingira yenye bajeti isiyotosheleza au yasiyokuwa na bajeti kabisa kwa ajili ya mafunzo endelevu kazini. Hii ina maana kwamba wakufunzi wa walimu wengi hawana maarifa ya sasa yenye msingi wa ushahidi na mbinu za kufundishia katika nyanja zao.⁴⁴ Kadiri programu za mafunzo ya ualimu zinavyoongeza urefu na viwango nya shahada za programu zao, ndivyo kunakuwa na shinikizo kubwa la kuajiri wakufunzi wa walimu wenye shahada za juu.⁴⁵ Matokeo yake, wakufunzi wa walimu wanazidi kuwa na uwezekano mdogo wa kuwa na uzoefu wa kufundishia ngazi ya msingi.⁴⁶ Mwisho, taasisi zinazotoa programu za mafunzo ya ualimu, kwa ujumla zinakosa hadhi na rasilimali za kutosha, hivyo kuwawia vigumu wakufunzi wa walimu kutoa na kuonesha ufundishaji wenye kiwango bora.aji wao.⁴⁷

Kuimarishe Uendelezaji wa Walimu nchini Zambia

VVOB, NGO ya Ubelgiji, kwa sasa inafanya kazi ya uendelezaji wa walimu katika nchi kumi. Nchini Zambia, VVOB inafanya kazi na taasisi zinazoendesha mafunzo ya walimu, zikiwemo Chuo Kikuu Chalimbana, Chuo cha ualimu Kitwe, na Chuo cha Elimu Sirenje, ili kuingiza mambo yafuatayo katika mtaala wa walimu wa nchi hiyo: (1) kazi za vikundi, (2) usimamizi wa darasa, (3) kufundisha kwa kuzingatia viwango nya wanafunzi, (4) utengenezaji na utumiaji wa zana za kufundishia na kujifunzia. Juhudi hizi zinasaidia kuondoa mikabala ya ufundishaji wa kizamani ya "kuzungumza na chaki".



VVBO inawasaaidia wakufunzi wa walimu kukuza ujuzi wa unasihi unaohitajika kusaidia na kuimarishe vipengele vipyta mtaala na mbinu na kujifunzia zinayomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji mionganoni mwa walimu tarajali.⁵¹



Ingawa kumekuwa na afua chache zilizotathminiwa kwa kina zinazohusisha mafunzo ya wakufunzi wa walimu katika eneo la KKK. Tafiti kadhaa zimeonesha kuwa huu unaweza kuwa mwelekeo wenyewe matumaini. Mafunzo kazini nchini Nigeria,⁴⁸ Ethiopia,⁴⁹ na Kambodia⁵⁰ yameonesha kuwa mafunzo yanaweza kuimarisha maudhui na maarifa ya mbinu za ufundishaji mionganoni mwa wakufunzi wa walimu; Utafiti nchini Nigeria pia umebainisha kuwepo kwa ongezeko la maarifa na mielekeo inayohusiana na KK katika madarasa ya awali.

MAPENDEKEZO

- 1 Kutoa kipaumbele kwa uzoefu wa kitaaluma katika kuajiri.** Wizara za Elimu na vyombo vingine vyenye udhibiti au uangalizi wa mchakato wa uteuzi wa wakufunzi wa walimu wanapaswa **kuweka kipaumbele katika kuoanisha mafunzo ya kitaaluma na uzoefu wa kitaalamu kulingana na uteuzi wao maalum.** Wakufunzi wa walimu wa programu za skuli za msingi, wanapaswa wawe na shahada katika elimu ya msingi na wawe na uzoefu wa kufundisha wa miaka kadhaa katika skuli za msingi na yote haya yaoneshe tathmini chanya. Wakufunzi wa walimu wazuri wasio na shahada zinazohitajika, wapewe kipaumbele katika kupatiwa programu za shahada zinazohitajika ili kukidhi vigezo ya sifa hizi.
- 2 Kusaidia uendelezaji wa kitaaluma wa wakufunzi wa walimu. Wakufunzi wa walimu wanapaswa kupatiwa mafunzo endelevu kazini** ili waweze kuonesha mbinu za kufundishia zinazozingatia ushahidi na kuwapatia utaalamu unaotumika sasa katika kujenga msingi wa KKK. Njia mojawapo yenyeye ufanisi wa ghamama ya kufanya hivi ni kuwashirikisha wakufunzi wa walimu katika KKK katika mafunzo kazini, pamoja na walimu wa skuli za msingi. Ingawa ghamama inaweza kuwa kikwazo kwa mafunzo ya mara kwa mara ya mtu mmoja mmoja, matumizi ya vifaa kama vile simu na vishikwambi yanaweza kutoa fursa kubwa katika ukuaji wa kitaaluma, kama vile awamu za mafunzo kwa njia ya mtandao. Juhudi za mafunzo masafa zimeongezeka mwaka 2020 na 2021 kutokana na janga la Uviko 19, na ushahidi kuhusu ufanisi wake unaweza kupatikana hivi karibuni.
- 3 Kutoa vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia.** Taasisi zinazotoa mafunzo ya ualimu lazima zipatiwe vifaa vya kutosha katika kiwango kinchohitajika kufanikisha ujifunzaji na ufundishaji bora. Vifaa hivi vijumuvishe, vitabu vya kisasa vya kiada vya madarasa ya awali na mitaala, vitabu vya kusoma vya watoto, vifaa vya kusomea Hisabati (vihesabio, vichezeo vya kupanga, n.k) kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia KKK, vifaa muhimu vya kidijitali, vitabu vya rejea, Miongozo ya walimu pamoja na maandalio ya somo, na majorida ya kiolectroniki yenyemada za utafiti kuhusu KKK.

Kuboresha uchaguzi na upangaji wa walimu wapya

Uchaguzi na upangaji wa walimu wapya katika skuli huchukuliwa kama mwanzo wa taaluma ya ualimu na uchaguzi na upangaji wa wanafunzi katika vuyo vya ualimu huashiria kuanza kufundisha. **Sera za uchaguzi na upangaji, pamoja na sera nyengine za usimamizi wa walimu huathiri ubora wa walimu wanaovutiwa na taaluma hii.**⁵² Sera hizi zinaweza kuathiri mitazamo kuhusu taaluma au ualimu ingawa zipo nje ya uwezo wa taasisi zinazoendesa mafunzo ya ualimu. Tafiti zinaonesha kwamba walimu tarajali walioingia katika mafunzo ya ualimu kwa kukosa sifa katika taaluma walizokuwa wakizipenda hypoteza ari ya kujifunza na kufanya kazi ya taaluma yao, pia hawaridhishwi sana na kazi yao ya ualimu.⁵³

Sera zinazosababisha ucheleweshaji wa muda mrefu wa upangaji au uzingatiaji mdogo wa mapenzi ya mwalimu kwa kazi yake zinaweza kuzuia wanaohitaji kuijunga na fani ya ualimu kuingia kwenye programu za mafunzo ya ualimu au kubakia katika taaluma baada ya kuhitimu mafunzo yao. Sera za uchaguzi na upangaji wa walimu pia zina athari kwa bajeti za kitaifa kwani mishahara ya walimu mara nyingi huchukua sehemu kubwa zaidi katika bajeti za elimu katika nchi za kipato cha chini na cha kati.⁵⁴ Nchi nyingi za kipato cha chini na cha kati zinakabiliwa na mvutano unaotokana na haja ya kuajiri walimu zaidi wenyewe sifa. Kwa mfano, Tanzania ingehitaji kuajiri walimu wapya zaidi ya 130,000 wa skuli za msingi ili kukidhi uwiano rasmi wa mwanafunzi na mwalimu, yaani mwalimu mmoja kwa kila wanafunzi 40 wa darasa la kwanza hadi la nne.⁵⁵ Mahitaji hayo makubwa ya walimu wapya yanaweza kuathiri uwezo wa taasisi zinazotoa mafunzo ya ualimu katika kuhakikisha wanafikia vigezo na viwango vya juu wakati wa uombaji wa kuijunga na mafunzo ya ualimu. Hii ni kwa sababu wanaweza kupata shinikizo la kuzalisha idadi ya kutosha ya wahitimu bila kujali uwezo wa taasisi husika katika udahili wa walimu wanafunzi.⁵⁶ Vikwazo vya bajeti vinavyopunguza uajiri wa watumishi wa umma pia huleta changamoto kwa kupeleka idadi ya kutosha ya walimu katika skuli baada

Ulimwenguni, zaidi ya walimu milioni 69 wa ziada watakuwa wanahitajika ifikapo 2030 ili kufikia Lengo la Nne la Maendeleo Endevu, linalohusu utoaji wa elimu bora kwa wote.





ya kuhitimu mafunzo ya ualimu.⁵⁷ Kuajiri walimu nchini Zambia na Malawi kumekuwa kukifanyika kwa kiasi kidogo na polepole na hivyo kuchukua miaka mingi tangu kuhitimu kwa walimu tarajali hadi kufikia kuajiriwa.⁵⁸ Mivutano hii ya kisera lazima ishughulikiwe na ngazi za juu za serikali ili kuhakikisha malengo ya elimu yanatengewa fedha za kutosha ili kuyafikia na pia nguvu kazi ya walimu inakidhi mahitaji ya nchi. **Zaidi ya walimu milioni 69 wa ziada watakuwawanahitajika ulimwenginu kote ifikapo 2030 ili kufikia Lengo la Nne la Maendeleo Endevu , linalohusu utoaji wa elimu bora kwa wote.**⁵⁹

Katika kukabiliana na mashinikizo haya, baadhi ya nchi za kipato cha chini na cha katil, ikiwa ni pamoja na Eritrea, Msumbiji, na Mali, ziamaejiri walimu wa mikataba ya muda mfupi badala ya walimu wa kudumu.⁶⁰ Ingawa mbinu hii inapunguza gharama, lakini pia inaweza kuwa na athari hasi kwa maoni ya walimu tarajali katika taaluma ya ualimu.⁶¹ Kwa hakika, kulingana na utafiti mmoja uliofanywa katika nchi 23 za kipato cha juu (OECD), watoto wenyewe umri wa miaka 15 wenyewe ufaulu wa juu wangependelea zaidi kuwa walimu katika nchi ambazo walimu wana mishahara mikubwa zaidi na wanafurahia hadhi kubwa wanayopewa katika jamii.⁶² Katika nchi za kipato cha chini na cha katil ambapo kwa ujumla walimu wanalipwa mishahara midogo,⁶³ hili limekuwa ni kikwazo kinachochangia waombaji wengi wenyewe ufaulu wa juu kutokuvutiwa na taaluma ya ualimu, na inaweza kuwa na matokea hasi katika ari ya utendaji kazi.⁶⁴ Tunatambua kuwa mishahara ya walimu huchukua sehemu kubwa ya bajeti ya elimu na tuna uhalisia ni kiasi gani ya mishahara hiyo inaweza kuongezwa, lakini uteuzi wa walimu hauathiriwi tu na udogo wa mishahara bali pia hadhi ya taaluma ya ualimu kwa ujumla katika soko la ajira.

Nchi zinaweza kukumbwa na ukosefu wa usawa katika ajira za walimu hata kama idadi ya jumla ya walimu iko ya kutosha kwa mfano Indonesia.⁶⁵ Hii inatokana na upendeleo wa walimu kufanya kazi mijini na maeneo wenyewe fursa nzuri zaidi.⁶⁶ Aidha, walimu wa kike wanaweza kukumbwa na vikwazo zaidi kuliko wenzao wa kiume kutokana na uwezo wao wa kufanya kazi mbali na familia, katika maeneo wenyewe shida au katika kuishi peke yao.⁶⁷ Aidha, ushawishi wa kisiasa (ikijumuisha ushawishi kutoka kwa vyama vya walimu⁶⁸) na rushwa katika upangaji wa walimu vimeelezwaa kutokea katika nchi za kipato cha chini na cha katil.⁶⁹ Sababu za aina hii hufanya walimu wenyewe sifa kuondoka haraka kwenye maeneo ya kazi wenyewe changamoto, hivyo kuongeza nafasi ya kuwa na walimu bora kati ya vijijini na mijini, hatimaye kuathiri matokeo ya elimu kwa ujumla.

Sera za uchaguzi na upangaji zinaweza kuingiliana na mafunzo ya ualimu katika kupelekea ama upatikanaji wa elimu bora na ya viwango vya juu kwa watoto wote, au kinyume chake kwa kupelekea athari mbaya katika sekta ya elimu. Katika nchi zenyeye lugha nyingi, kwa mfano, lugha ya kufundishia katika skuli za msingi, taasisi zinazotoa mafunzo ya ualimu, na sera za upangaji vinaweza visiwe vinaendana. Mwalimu anaweza kuelewa umuhimu ya ufundishaji wa wazi wa kusoma na kuandika, inaweza kuwa vigumu kutekeleza aina hii ya ufundishaji kwa kutumia lugha ambayo mwali muhaifahamu. Kutoendana kati ya uwezo wa lugha wa mwali muhaifahamu, uzoefu kutoka katika mafunzo, lugha ya kufundishia inayotumika katika eneo linalohusika na sera za upangaji wa walimu wapya kunaweza kupunguza ubora wa elimu wanayopatiwa watoto.⁷⁰ (Tazama maelezo zaidi katika LOI How-To-Guide kuhusu changamoto za ufundishaji wa stadi za KKK.

MAPENDEKEZO

